

# TANGAZO LA KAZI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA



**NAFASI ZA KAZI – TAREHE 26/03/2018.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA  
IRAMBA ANAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI KWA WANANCHI  
WOTE WENYE SIFA ZA KUJAZA NAFASI:**

### **1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III NAFASI 34**

#### **a) Sifa za Mwombaji.**

Mwenye Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo. Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya jamii na Sanyansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **b) Kazi na Majukumu**

- Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu.

- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa Kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- Ngazi ya mshahara TGS B.

Waombaji wote wawasilishe CV, Picha mbili za passport size za hivi karibuni na vyeti vya Shule na taaluma vikiwa vimethibitishwa na wakili anayetambulika.

Mambo Muhimu ya Mwombaji ambayo anapaswa kuyazingatia.

- (i) Lazima Mwombaji awe Mtanzania
- (ii) Mwombaji awe hajawahi kufungwa, kupunguzwa au kufukuzwa kazi Serikalini.
- (iii) Mwombaji awe na Umri wa Miaka 18 hadi 45.
- (iv) Barua za maombi ziambatane na Vivuli vya Vyeti vya Taaluma, picha mbili (2) passport size za rangi za hivi karibuni, Maeleo binafsi (CV) yakionyesha anuani Kamili, wadhamini watatu, namba za simu za Mwombaji.
- (v) Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe na uthibitisho kutoka baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) na NACTE (Baraza la Elimu ya Ufundji Tanzania)
- (vi) Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo

**NB:** Ni kosa la Jinai kuwasilisha cheti cha kughushi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya muhusika.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 155,  
**KIOMBOI/IRAMBA.**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 09/04/2018 saa 9:30 alasiri.



Engelberth B. Kalekona  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
IRAMBA.**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA IRAMBA*